

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA

10 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 10 JUNI, 2015

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA:

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha, 2013/2014 (*The Annual Report of the Bank of Tanzania for the Year 2013/2014*).


The Annual Performance Evaluation Report for the financial Year 2013/2014

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

178. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Barabara ya Ilolangula – Isebya – Nyashinge – Mto Nyikonga hadi Rwamgasa ni kiungo muhimu cha shughuli za Kiuchumi kati ya Wilaya za Mbogwe na Geita:-

- 
- (a) Je, ni lini Serikali itaongeza fedha zaidi katika kujenga na kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo;
 - (b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika Mto Nyikonga.

179. MHESHIMIWA MENDRAD LUTENGANO KIGOLA (MUFINDI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia maeneo mbadala Wananchi wa Vijiji vya Sawala, Kihanga, Luhunga, Mikonge, Igoda, Mininga, Kitasengwa, Iyegaya, Kilolo, Ihomasa na Udumka ambao maeneo yao yalichukuliwa na Kampuni ya **MPM**, *Uniliver Tea* na Idara ya Misitu kwa ajili ya kilimo cha chai na upandaji miti na kusababisha Wananchi hao kukosa maeneo kwa ajili ya kilimo, ufugaji, na ujenzi wa nyumba za kuishi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

180. MHESHIMIWA SUSAN LIMBWENI KIWANGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kata ya Mlimba ni kubwa sana na hivyo kustahili kuwa Jimbo la Uchaguzi linalojitegemea:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Mlimba ili kuondokana na kero ya kuazima majengo ya TAZARA ambayo bado hayakidhi mahitaji ya Kituo cha Polisi.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

181. MHESHIMIWA SABREENA HAMZA SUNGURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Kwa mujibu wa utaratibu mpya wa malipo ya madhuhuri yote Mahakamani yanapaswa kulipiwa benki ya NMB; utaratibu huo umeanza mwezi Aprili, 2015 kwa tangazo la Mtendaji Mkuu wa Mahakama lakini pamoja na nia hiyo nzuri utaratibu huu umegeuka kuwa kero kwa Wananchi wa vijijini ambako hamna huduma ya benki na pia hulazimika kulipa ada ya kuanzia Tshs. 1,500/= na kuendelea:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza kero hiyo kwa Wananchi walioko vijijiini.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

182. MHESHIMIWA JOHN PAUL LWANJI (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali kuitia REA, iliahidi kupeleka umeme Mwamagembe katika mpango wake wa awamu ya pili (PHASE II) Wilayani Manyoni:-

Je, ni lini mpango huo utatekelezwa ili Wananchi wa Mwamagembe wapate umeme kabla ya Juni 2015 kama ilivyoahidiwa.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

183. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Zipo taarifa kwamba kuna upungufu wa Wataalam wa Mionzi (Radiologists):-

- (a) Je, kuna wataalam wangapi katika nchi yetu;
- (b) Je, masomo ya kozi hiyo ni ya muda gani.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

184. MHESHIMIWA RITTA ENESPER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:-

Je, ni shule ngapi na vyuo vya elimu hapa nchini ambavyo vimeruhusiwa kutoza ada kwa fedha za kigeni.

**DODOMA
10 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**